شَجَرة الدِّين
هَدِيَّةٌ للمُهتَدِين

MTI WA DINI, ZAWADI KWA WALIOONGOKA KATIKA DINI

(Mizizi na matawi ya dini)

Mambo muhimu anayofaa kuyajua muislamu

Toleo la 1

USTADH
ALI ALHAIDARY
(AL-MUFATTISH)

شَجَرة الدِّين

هديَّةٌ للمُهتَدِين

MTI WA DINI, ZAWADI KWA WALIOONGOKA KATIKA DINI

(Mizizi na matawi ya dini)

MAMBO MUHIMU ANAYOFAA KUYAJUA MUISLAMU

(TOLEO LA 1)

USTADH
ALI ALHAIDARY
(Al-mufattish)

Utangulizi

Bismillahi rwahmani rwahiim, kila sifa njema ni za Mwenyezimungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu, na swala pamoja na salamu zumuendee mtume wetu kipenzi Chetu Muhammad pamoja na familia yake na maswahaba zake na wafuasi wake wote kwa jumla

Hakika nimejikalifisha kuandika kijitabu hiki huku nikijitahidi ingawa mimi si katika wale wanaostahiki kuwa watunzi wa vitabu katika dini yetu, kwa kuzingatia uchache wa Ilimu yangu na udogo wa uchaji Mungu wangu ukilinganisha na walivyokuwa watunzi walionitangulia ambao ni mahodari wa utunzi na bahari katika ilimu ya dini, ambao ndio tunaowategemea katika kuchukua ilimu na kuchukua maana ya maneno aliyo yasema Mwenyezimungu katika kitabu chake kitukufu cha Quruani na hadithi(maneno) za Mtume wetu muhammad (S.A.W), kwani si kila mtu anaweza kuelewa maneno ya Allah wala ya mtume Muhammad(S.A.W) isipokuwa wale wanazuoni wetu wanaotegemewa.

Kitabu hiki cha " Mti wa dini zawadi kwa walioongoka katika dini" ni kijitabu kidogo nilichokusudia Muhtadeen yaani waongofu ambao wanataka kujua ilimu yao ya dini ili waweze kumuabudu mwenyezimungu anavyostahiki kuabudiwa.

Natarajia atakae kisoma kijitabu hiki na kukielewa basi atakuwa ni miongoni mwa wale wenye ufahamu kwenye dini na ataweza kuwasomesha na wenzake haswa wale ambao wamesilimu karibuni na hawajapata nafasi ya kuijua dini yao ki ukamilifu haswa upande wa ibada.

Namuomba Mwenyezimungu ajalie thawabu hizi ziende kwa bwana mtume Muhammad na ziwafikie kila aliekuwa kwenye msururu wa kupokea mafunzo yake na kuyasomesha mbeleni makarne hadi makarne hadi ikawafikia walimu watu na hadi ikatufikia na sisi, basi Allah ajalie baraka ziwe kwa wote hao, na wale waliotuzaa ,na wale waliotupenda na wale waliochangia katika kuandika na wale waliokisoma na wale waliokisomesha zaidi.

Kitabu hiki tumeanza na tolea la Kwanza na natarajia in sha Allah kitaendelea na toleo La pili na zaidi ya hapo ili in sha Allah kidogo kidogo tuwe tumechanganya ilimu yote ya dini kwa jumla. Kwa hivyo, mwisho wa kitabu hiki sio mwisho wa ilimu ya dini ya Kiislamu bali ndio mwanzo wa kufungua utamu wa ilimu ya dini ya kiislamu ambayo Ni bahari kuu isio na mwisho iliojaa kila aina ya mapambo mithili ya lulu na marijani.

Miongoni mwa vitabu tuliotoa maelezo na kuyaweka hapa ni kitabu cha : risala , safina, Duraru, muqaddimatul khadhramiyyah , mabadiul fiqhiyya, attaqriraatul sadiidah,fat-hul-muin , lubbu lubaab na venginevyo Vilivyotungwa kwa kiarabu.

Allah ajalie kwenye mizani ya amali zetu njema kama alivyosema kwenye quran :

وَمَا تُقَدِّمُوا لِأَنْفُسِكُمْ مِنْ خَيْرٍ تَجِدُوهُ عِنْدَ اللَّهِ هُوَ خَيْرًا وَأَعْظَمَ أَجْرًا وَاسْتَغْفِرُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ

(Na kheri yoyote mnayo itanguliza kwa ajili ya nafsi zenu mtaikuta kwa Mwenyezimungu , imekuwa Bora zaidi, na ina thawabu kubwa sana, na mtakeni mwenyezimungu msamaha, hakika mwenyezimungu Ni mwenye kusamehe.

Mimi kijana wenu faqir:
Ustadh Haidar Abdulwaheed Ali
Kwa jina maarufu Almufattish Ustadh Ali Alhaidary kutoka Malindi Kenya.

DINI YA KIISLAMU

USULI YA DINI

Ama usuli ya dini(mizizi)ni mitatu,bila ya mizizi hii uthubutu wa uislamu kwa mja atakuwa haujakamilika

Nayo ni: 1)Ihsan

2)Islam

3)Iman

1) Mlango wa Ihsan

Ihsan ni **kumuabudu Allah (Mwenyezimgu) kama kwamba wewe unamuona yeye,na ikiwa (akakupitia kwenye akili kuwa) humuoni yeye basi (juwa)yeye (Allah) anakuona wewe**.

2) Nguzo za kiislamu

Haya ni mambo yanapokamilika na kupatikanwa kwa mtu huwa amekuwa muislamu kamili.

Nayo:

1. Shahada
2. Swala
3. Zakkah
4. Saum ya Ramadhan
5. Hajj(kwa mwenye uwezo wa kuenda makka)

a) Shahada

Ndio nguzo ya kwanza ya kiislamu nayo ni kusema (ASH HADU AN LAA ILAHA ILLA LLAH WA ASH HADU ANNA MUHAMMADAN RASULU LLAH)

أشهد أن لا إله إلّا الله وأشهد أنّ محمدا رسول الله

N/B- Mtu akitaka kuslimu lazima asema maneno haya,anaposema haya ashakuwa muislamu,hata bila kutafuta shehe amsilimishe, ingawa akitafuta shehe atapata na baraka na kuombewa mungu na watu watajua kuwa ni muislamu.

Mtu anapo silimu atakikana ajifakhiri kuwa ni muislamu wala asiogope kuenda msikiti au kuvaa nguo za kiislamu, kumbuka uislamu ni dini ya watu wote kwa hio na wewe pia ni miongoni mwao, jifakhirinnao na uwajulishe watu kusilimu kwako

Ni vizuri mtu kukiriri shahada ili ajenge upya uislamu wake.

b) Swala

Swala zinafaa ziswaliwe zote kwa vipindi vitanu.Atakae acha kuswali basi huyo ni kafiri na atapata dhambi. Hata ukiwa popote pale usiache swala.

vipindi vya swala ni: kila swala ina wakati wake maaluum wa kuswali unaweza kuswali wakati wowote kuanzia mwanzo wa kipindi hadi mwisho,

amma kipindi kikiisha itabIdi uswali hivyo hivyo na utapata dhambi.

*Utaweza kujua wakati wa swala kupitia adhana ya msikitini (isipokua alfajiri adhana inakuwa mbili, na ile ya kwanza huwa kipindi cha swala BADO hadi adhana ya pili ndio wakati wa swala utakuwa umefika., au pia unaweza kudowload programu za nyakati za swala katika simu yako.Ni muhimu kujua kwamba kila mji una wakati wake tofauti na mji mwengine kama utatumia saa ya standard, au pia unaweza kutumia mwenendo wa jua kama vile jedwali linavyoelezea.

Jina la swala	**Muda wake**	**Rakakaa kiarabu**	**Rakaa kinambari**
Asubuhi/ fajri	Kuanzia kuchomoza muangaza mweupe upande wa kuchomoza jua—**mwisho wa kipindi** ni pindi linapochomoza jua.	Rakatein	2
Adhuhuri	**Mwanzo wa kipindi** ni jua litakapo pinduka kutoka katikakati ya mbingu(mchana) na kuanza kuelekea upande wa magharibi --- **mwisho wa kipindi** ni kivuli kuwa urefu sawa na kitu(object) iliozaa kivuli na nyongeza kidogo ya kivuli cha utosi	Arbaatu rakaati	4
Alasiri	**Mwanzo wa kipindi** ni Inapomalizika kipindi cha adhuhuri –**mwisho wa kipindi** ni jua kuzama	Arbaatu rakaati	4
Maghabirui	**Mwanzo wa kipindi** -Baada ya jua kuzama- **mwisho wa kipindi** hadi yapotee mawingo mekundu upande wa magharibi	Thalath athatul rakaat	3
Isha	**Mwanzo wa kipindi** ni pindi inapomalizika kipindi cha magharibi--- na **mwisho wa kipindi** ni kuanza kutoka muangaza mweupe upande wa mashariki wakati wa alfajiri	Arbaatu rakaati	4

Sababu za kukosa kuswali.

Katika uislamu hakuna sababu ya kumfanya mtu asiswali isipokuwa mwanamke mwenye hedhi au damu ya nifasi kama itakavyo elezewa mbeleni.

Amma wengine wote maadamu mtu amebaleghe si mtoto na ana akili si mwendawazimu, basi swala inamlazimu na ataswali kwa uwezo wake ikiwa hawezi kuswali kwa kawaida. Kwa mfano, mtu ambae ni mgonjwa basi ataswali kwa kadri anavyoweza imma kwa kukaa, akishindwa basi kwa kutegemea na akiwa hawezi basi kwa kujilaza ikishindikana basi kwa kutumia kidole na hatimae kwa kuashiria kupitia jicho au kwa kuswali kupitia moyo. Ilimradi mwanadamu asikate mawasiliano yake na mola wake kwa sababu swala ni njia ya mawasiliano beina ya mja na mwenyezimungu na mtu hafai kukata mawasiliano na muumba wake kwa hali yoyote atakayokuwa.

Hali mbili mtu kama hajaswali hapati dhambi

1. Mtu aliekuwa amelala hadi kipindi cha swala kikapita basi mtu huyo akiamka wakati wowote ule ataswali wala hapati dhambi. Isipokuwa mtu hafai kulala wakati anajua kwamba wakati wa swala hauko mbali na lau atalala basi wakati wa swala utampita bila yeye kuswali.

2. Mtu aliesahau kwamba ni wakati wa swala hadi kipindi cha swala kikampita basi mtu huyo akikumbuka ataswali wala hatopata dhambi.

Swala haiwezi kukamilika hadi masharti yote ya swala yakamilike , nayo ni kama yafutayo

Masharti ya kuswihi swala

i. Lazima uwe Muislamu.
ii. Uwe umesafishika na hadathi kubwa na ndogo
iii. Uwe tahara(safi) kutokana na najisi muilini,nguoni na sehemu yakuswalia
iv. Kustiri uchi
v. Kuelekea kibla(kuelekea Al-kaaba ilioko mjini makka arabuni)
vi. Wakati wa swala uwe umeingia
vii. Kujua kuwa swala ni faradhi ,Na kutofikiria kuwa nguzo za faradhi za swala kuwa ni sunna

Maelezo zaidi kuhusu masharti ya swala

Tahara ya hadathi

Hadathi ni hali ya kutokuwa safi (kimaana) baada ya kutokea hali fulani (muilini)

Hadathi imegawanyika mara mbili.

- ✓ Hadathi Kubwa
- ✓ Hadathi Ndongo

Hadathi Kubwa

Ni hali ambayo ambayo ikikufikia ni lazima uoge (muosho wa sharia)

Mambo yanayomlazimu mtu kuoga

1) Kustarehe beina ya mume na mke kadri ya kuingiza kichwa cha tupu ya kiume katika tupu ya mwanamke.(wote wataoga) **hii hali huitwa janaba**.
2) Kutokwa na manii[1] imma usingizini au hali yoyote nyengine ilehata kama ni kwa kuota ndoto .
   n/b : ukitokwa na madhii[2] au wadii[3] si lazima uoge utaosha tu ile nguo yako na tupu yako ya mbele.
3) Baada ya damu ya hedhi kukoma kwa mwanamke
4) Baada ya damu ya nifasi(uzazi) kukoma kwa mwanamke
5) Baada ya kuzaa
6) Baada ya mtu kufariki(ataogeshwa) ili akazikwe

[1] Manii ni maji ya uzazi,harufu yake ni kama harufu ya madonge ya mahamri,na yana mtelezo

[2] Ni maji mepesi yanayotoka mtu anapofikiria tendo la ndoa,huwa ni rangi ya maji na hutoka kidogo,utasafisha kwa kupangusa kwa maji tu.

[3] Majii mazito yanayotoka baada ya kumaliza kutoka mkojo

Jinsi ya kuoga (muosha wa sharia)

1) Kueka nia(moyoni) kuwa waoga kuondosha janaba.
2) Kueneza maji[1] muili mzima: anza kuosha mikono miwili kabla ya kuyaingiza katika chombo cha kutekea maji,halafu uta osha nywele mpaka zote zipate maji hadi mizizi,halafu utachukua chombo cha maji na utamwagilia upande wa kulia ,utajisugua ili ngozi yote ipate maji,utajimwagilia upande wa kushoto kama vile ulivofanya kulia,utajisugua mikono mpaka mikono na ngozi zilizofichika kama vile ndani ya maskio,utajimwagilia tena maji kwanzia kichwani ili yamwagike muili mzima.(usitie sabuni wala chochote, maji yatakikana yawe safi bila mchanganyiko)…baaada ya hapo utakuwa umemaliza kuoga na baada ya hapo kama utatataka kutia sabuni atajipaka sabuni

Hakikisha unapooga maji hayarudi ndooni,yaani unaweza kuteka maji halafu usongee mbali kidogo ndio ujimwagilie maji.Ukipiga mbizi baharini au mtoni,ama pia ukiwa na mfereji wa juu (shower) ni bora zaidi.

Mambo ambayo mtu akiwa na janaba hafai kufanya

1)Kuswali 2)kusoma Qur-an
3)kutufu(kuzunguka Al-kaabah) 4)kubeba msahafu (Qurani)
5) Kuugusa msahafu 6)kukaa msikitini

Mambo ambayo mwanake akiwa na hedhi na nifasi hafai kufanya

1)Kuswali 2) kusoma Qur-an
3)kutufu(kuzunguka Al-kaabah 4)kubeba msahafu (Qurani)
5)kutenda tendo la ndoa[2] 6)kukaa msikitini
7)kupita pita msikitini akichelea kuchafua msikiti kwa damu
8) kufunga swaum 9)kupewa talaka (na mume wake akimpa-talaka basi talaka itakuwa imeswihi ingawa mume atapata dhambi)

Mambo ambayo mtu akiwa ana hadathi ndogo(hana udhu) hafai kufanya.

1)Kuswali
2)kutufu(kuzunguka Al-kaabah) 3)kubeba msahafu (Qurani)
4) Kuugusa msahafu

[1] Maji ya kuogea na kuondoshea najisi tizama ukurasa

[2] Mwanamke hafai kustarehe na mume wake kupitia tupu yakemwanamke ya mbele wakati wa hedhi) wala kucheza cheza beina ya magoti na kitovu, ila mengine yafaa ,kumbuka kustarehe nae kwa kupitiatupu ya nyuma ni HARAM

Hadathi ndogo

Ni hali ambayo ukiwa nayo hufai kuswali mpaka utawadhi

Kutawadha(udhu)

Ni kuosha viungo maalum vilivyowekwa na sheria kwa kutia nia.

Jinsi ya kutawadha

1) **Kuweka nia***
2) Kuosha viganja vya mikono
3) Kupiga msuaki
4) Kusukutua(kutia maji mdomoni na kutema)
5) Kupandisha maji puani
6) Kupiga Bismillahi
7) **Kuosha uso**(kuanzia sikio la kulia hadi la kushoto na kidevuni pamoja na ndevu hadi kwenye mwanzo wa nywele za bapa)[1]
8) **Kuosha mikono miwili hadi kwenye viwiko viwili.**
9) **Kupangusa badhi ya kichwa (nywele au ngozi)**
10) Kuosha maskio
11) **Kuosha miguu hadi macho ya miguu**
12) **Kufuatanisha kimpangilio kuanzia no1 hadi mwisho**

Mambo yananayo vunja udhu (kuharibu)

1) Kutokwa na kitu chochote kupitia njia: tupu mbili ya mbele au ya nyuma hata kama niupepo
2) Kupoteza fahamu ima kwa kulala au kuzimia au kwa hali yoyote ile,iwe niulevi au mambo mengine ila Kulala huku makalio yako yametulia ardhini. (mtu akisinzia udhu wake uko ni hadi alale yaani usingizi wa kukosa fahamu)
4) Kugusana mwanamke na mwanamume ambao wanaweza kuoana (yaani si wanafamilia wa karibu ambao hawafai kuoana) wote wakubwa walio baleghe bila kizuizi chochote[2]
5) Kugusa tupu ya binadamu kwa matumbo(mbele) ya vidole au matumbo ya yaviganja[3]

n/b- mtu ambae anatokwa na mikojo au chochote kila wakati hata akijizuia , basi mtu atasubiri hadi kipindi cha swala kifike halafu atajisafisha na atabadilisha nguo iliogusa mkojo na atatawadha na ataswali hata kama mikojo itamtoka huku anatawadha au kuswali

[1] Utaanza sikio la kulia,bapa,sikio la kushoto na mwisho kidevuni
*hizo zilizokolezwa wino ni faradhi yaani ni lazima

[2] Kizuizi cha kuzuia ngozi zisigusane, amma kugusana jino au nyele au kucha haina neno. Pia mkeo anakuvunjia Udhu ukimgusa

[3] Iwe ni tupu ya mbele au nyuma,(hata kama ni yako) au ya mwanao au ya binadamu iliokatwa.

Tayammamu

Ni hali ya kutumia mchanga badala ya maji kuondosha hadathi kubwa au ndogo

Mambo yanayopelekea kutayammam

I. Kukosekana maji au maji yawe kidogo kadri ya kutumia nyumbani na kunywesha wanyama wenye cheo(mifugo na mbwa wa kulinda)
II. Kuhofia maji kuwa yatakudhuru kwa sababu ya maradhi Fulani
III. Njia ya kwenda kutekea maji kuwa ni hatari haipitiki(ima kuna majambazi au wanyama Hatari)
IV. Maji kuwa ghali (kwa aliesafarini)

Jinsi ya kutayammum

a) Utakusanya mchanga viduru viwili Visafi
b) Utagonga duru la kwanza kwa viganja vya mikono na upanguseusoni
c) Utagonga kile kiduru kengingine na upanguse (lilevumbi)kwenye mikono miwili hadi kwenye viwi viwili

n/b kugonga viganja vya mikono miwili kabla ya kupangusa ni bora ili upunguze mchanga ulioko mkononi na kubakia na vumbi.

Mambo yanayovunja tayammum

1. Kila kinachovunja udhu
2. Kuritadi(kutoka katika uisilamu- Mwenyezimungu atulinde na Kitendo hiko)
3. Kupatikana maji ikiwa umetayammum kwa kukosekana maji.
4. Kuisha kwa udhuru kama vile kupona maradhi
5. Kuisha kipindi cha swala ya Faradhi

Najisi

Ni vitu visokuwa safi ambavo si vizuri kukaa muilini,nguoni au mahala popote hata kama ni nyumbani au garini, na haikubaliki swala mpaka viondolewe kwenye nguo ya mwenye kuswali ,au muili wake au sehemu anayoswalia.

Aina za najisi.

1. Najisi nzito
2. Najisi nyepesi
3. Najisi ya kati na kati

1 Najisi nzito

Nayo ni mbwa[1] na nguruwe na nyama yao na mate yao na mikojo na kinyesi chao na kitakacho zaliwa na wao,hata kama mzazi mmoja atakuwa si mbwa wala nguruwe, na kila kitu chao hata kama ni nywele.

Jinsi ya kusafisha najisi nzito

Ni kuosha sehemu uliogusana na najisi mzito mara saba.kwa kutumia maji safi. katika hizo mara saba , mara moja iwe ni kwa mchanga baada ya kuondosha hio najisi.

2) Najisi nyepesi

Ni mkojo wa mtoto wa kiume chini ya umri wa miaka miwili na ambae hajalishwa chochote ila maziwa tu.

Jinsi ya kusafisha najisi nyepesi

Ni kunyunyiza sehemu ilokuwa na najisi kwa maji safi.

3) Najisi ya katinakati

Ni chochote kinachotoka katika tupu mbili ya mnyama au binadamu(mkojo,kinyesi, madhii,wadii) ila manii na mayai, maiti/mizoga zote pamoja na ngozi zakwe, na mifupa, Ila maiti ya (binadamu,samaki au nzige),matapishi,tembo,damu,usaha, maziwa ya mnyama asieliwa, kipande kilichokatika kutoka kwa mnyama hai hata kama ni ngozi au nywele,

[1] Iwe ni ngozi yake majimajimaji,mate au chochote kile kinachotoka katika wanyama wawili.

Jinsi ya kusafisha najisi ya kati na kati

Utaiondosha najisi,halafu utaosha pale palipogusana na najisi hadi iondoke rangi yake,harufu yake au ladhayake.kwa kutumia maji safi bila sabuni.

*Ikishindikana na kubakia moja katika sifa zake tatu ima rangi, harufu au ladha itakuwa haina neno. Lakini zikibakia sifa mbili utaendelea kuosha .

N/B – unapotaka kusafisha mkojo ambao uko sakafu ya simiti ni bora ufute ile najisi hadi upotee yote kabla ya kutia maji na baadae ndio utie maji na upanguse, na baadae upanguse na kitambaa chengine safi

Kama ni ardhi imemwagikiwa na najisi utaimwagilia maji safi ya kiasi zaidi ya najisi ili ile najisiizame.

Ngozi[1] ya mnyama alie maiti inasafishika ikipakwa rangi au kemikali Ya kuondoshea bacteria na vipande vya nyama vilivyoganda ngozini Mfano rangi inayowekwa katika ngozi ya viatu.

Kuchamba/ kutamba

Ni njia moja ya kuondosha najisi ,nayo ni kusafisha tupu yako baadaya kwenda haja ima kubwa au ndogo. Mtu alienda haja bila kuchamba atahisabika ana najisi,na ni lazima achambe na aoshe sehemu ya nguo iliogusa najisi. Amma atavunja sharti la swala na swala haitakubalika.

Jinsi ya kuchamba/

Kujipangusa kwenye mzunguko wa tupu kwa kutumia mawe na maji au kama itashindikana hivo viwili na kukupelekea kuchagua kimoja basi maji ni bora zaidi.

Unapokosa maji unaruhusiwa kutumia jiwe au chenye sifa ya jiwe .

Masharti ya kutumia jiwe

1) Ni yawe ni mawe matatu.
2) Na yasiwe ni yenye najisi.
3) Mawe yasiwe maji maji
4) Na lisiwe ni dogo kadri ya kuweza kuzama kwenye tundu ya tupu.
5) Najisi isiwe imegura sehemu iliotoka
6) Isipandane na najisi nyegine

[1] Mnyama anaeliwa asipochinjwa akafariki kwa kugongwa au ugonjwa au kupigwa na mnyama mwenzake na Haikupatikana kuchinjwa basi ni maiti(mzoga) na kam amechinjwa basi haitwi maiti na si najisi. Amma mnyama Asieliwa akichinjwa anabaki kuwa vile vile maiti(mzoga) isipokuwa samaki na mzige na binadamu ndio maiti zao Si najisi.

Masharti ya kutumia chenye sifa ya jiwe.

1) Kitu katakachotumiwa kiwe ni kisafi
2) Kiweze kukaruza (kisiwe laini) kikaeneza najisi
3) Kiwe ni kikavu, kisiwe na maji maji
4) Kisiwe ni chakula.
5) Kisiwe ni najisi kama vile choo cha ng'ombe.
6) Kisiwe ni chenye kuheshimiwa kama vile koko ya chakula, kiguguta ama mfupa wa nyama.
7) Kisiwe ni chenye madhara kama vile upupu.
8) Kisiwe na thamani kama vile pesa au kitabu cha masomo

N/B-"Karatasi za chooni(toilet paper) inasifa ya jiwe.

Maji

Maji ni kitu cha muhimu katika dini ya kiislamu, hata mtumi Muhammad (salla llahu aleihi wa salam)[1] amesema "uislamu ni usafi jisafisheni, kwani hataingia peponi ila alie msafi."

Maji yamegawanyika mara tatu kulingana na hali ya usafi na matumizi yake, nayo ni ;

1) Maji Safi yasiyoweza kusafisha.
2) Maji Safi yanayoweza kusafisha.
3) Maji yalio najisika.
4) Maji yaliotumika kuondoshea hadathi au najisi.

1) Maji Safi yasiyoweza kusafisha.

*Ni maji yalioengezwa vitu visafi vikaharibu sifa ya maji ima rangi, ladha au harufu.kama vile sukari,sabuni au rangi , au chochote kile kilichosafi isipokuwa mchanga au chumvi ya bahari, amma chumvi ya mwawe basi pia itaharibu
*Aghalabu hayaitwi tena maji bali hugeuka jina mfano Chai, Soda, Kahawa pia Marashi.
Maji haya huwezi kuondosha najisi na pia huwezi ondoshea hadathi zote mbili kubwa au ndogo wala kuchambia, ingawa yatakuwa ni halali kupikia au kunywa au kusafishia nguo,au sehemu, muili usio na najisi

[1] Jina la mtumi likitajwa inatakikana useme hivo

2) Maji Safi yanayoweza kusafisha.

Ni maji yenye sifa kamili ya maji, na haya ndio maji pekee unayotakikana Kuondoshea najisi na kuondoshea hadathi kubwa na ndogo na kuchambia.
Asili ya maji yaliosafi ni:

a) Maji ya mvua
b) Maji ya mto
c) Maji ya ubaridi (umande)
d) Maji ya kisima
e) Maji ya bahari
f) Maji ya chemichemi
g) Maji ya theluji (snow)

n/b maji ya mabomba/mifereji yanatoka moja katika asili hizo kwa hio ni safi ya kuweza kusafishia

3) Maji yalio najisika

1.Ni maji yalioingiwa na najisi ndani yake yakawa chini ya daba mbili[1] (220 litre) takriban au 217 au 218 hata kama hayakugeuka.

2.Maji yalioingiwa na najisi yakawa au Zaidi ya daba mbili (kullatein-kipimo cha zamani cha arabuni) hadi yakageuka rangi au harufu au ladha. Mfano mto ugeuke uwe wa damu.

n/b maji yakiwa ni daba mbili /kullatein (220 L) na zaidi basi huwa hayanajisiki hata yakiingiwa na najisi mfano maji ya bahari au kidimbwi Isipokuwa yageuke kama tulivyoelezea hapo juu. ,tofauti na maji chini ya kiwango hiko ambayo tunayaita maji kidogo.

*Maji yelionajisika hayawezi kutumiwa kusafishia na chochote kitakacho gusa maji yalionajisika kitakuwa najisi na hadi kioshwe kama unavyoosha najisi.

*Maji yalionajisika ukimwaga kwenye maji mwengi ya kullatein na zaidi basi yote yatakuwa safi, amma maji ya kullatain na zaidi yakinajisika yanaachwa hadi yajisafishe yenyewe kupitia muda.

KUSTIRI UCHI

Muislamu anahimizwa kila mara asitiri uchi wake na pia haikubaliki swala ya mtu kama uchi wake hajausitiri vizuri . nguo ya kustiri uchi isiwe ni yenye kuonyesha rangi ya muili kwa mwanamume na kwa mwanamke pia, pamoja kwa mwanamke nguo isiwe ni ya kubana.

Uchi wa mwanamume ni tofauti na mwanamke.

A) Uchi wa mwanamume

Ni kuanzia kitovuni hadi chini ya magoti (kimbele na nyuma

B) Uchi wa mwanamke

Uchi wa mwanamke Katika swala Ni mwili mzima isipokuwa uso na viganja vyake vya mkono.

n/b Amma nje ya swala mwanamke akiwa na wanawake wenzake au na maharim zake (ambao hawawezi kumuoa) basi anafaa astiri beina ya kitovu na Magoti, illa kama kuna mwanamke asie muislamu au muislamu asie na tabia njema basi anafaa ajistriri muili mzima

* Amma kama ni nje ya swala basi asitiri muili wake mzima mbele ya wanaume wasiokuwa mahram illa mumewe.
* Mume na mke wanaruhusiwa kuonana uchi wao, isipokuwa wakati wa swala watajistiri kama tulivyoeleza.

NAMNA YA KUSWALI

1) **Kueka Nia**.
2) **Kupiga takbir ya kufungia swala (ALLAHU AKBAR.)**
3) **Kusimama (kwa mwenye uwezo.)**
4) **Kusoma Suratul FATIHA (AL_HAMDU.)**
5) **Kusoma aya am asura yoyote ya Quran**.
6) Kusema (ALLAHU AKBAR)
7) **Kurukuu (na kujituliza.)**
8) Kusema mara tatu. (sub-hana rabbiyal adhim wabihamdihi) katika rukuu
9) Kusema (Samiallahu liman hamidah)
10) **Kusimama na kujituliza**.
11) Kusema (ALLAHU AKBAR)
12) **Kusujudu na kujituliza katika sijda(viungo ambazo unaposujudu zinatakikana viguse ardhi ni, bapa la uso,viganja vya mikono miwili, magoti mawili na vidole vya miguu miwili.**
13) Kusema mara tatu (sub-hana rabbiyal aala wabihamdihi) katika kusujudu
14) Kusema (ALLAHU AKBAR)
15) **Kukaa baada ya kusujudu (na kujituliza.)**
16) Kusema (rabbi ghfirliiy warhamniy waafiniiy waafu anniiy
17) **Kusujuudu tena (na kujituliza.)**[1]
18) Kusema (ALLAHU AKBAR)
19) Kukaa attahiyatu ya kwanza (baina ya rakaa mbili.) tizama kurasa 16 jinzi ya kusoma
20) Kusema (ALLAHU AKBAR)
21) **Kukaa attahiyatu ya mwisho na kumswalia Mtumi.(Allahuma Swali Ala Muhammad Wa Ali Muhammad**)……..maelezo zaidi ukurasa 16
22) Kupiga salamu, kusema "Assalaam aleikum warahmatulla" (Ukianzia Kugeuza Uso Upande wa kulia na kisha kushoto na kusema tena salamu.
23) Kuzifuatanisha kimpangilio.

Maelezo zaidi kuhusu nguo za Swala

Niyyah

Ni nguzo katika nguzo za swala, nayo utasema "Nawaitu Uswalli Faradhati Swalaat……..Adhuhuri[a]…..Arbaata¨ rakaat[b] lillahi taala." Allahu Akbar ["Nanuia kuswali swala ya faradhi ya adhuhuri rakaa nne kwa jili ya mwenyezimungu alietukuka."][2]

---

[1] Ikifikia hapo huwa ndio inapoitwa raka moja, ukitaka kuenda kwenye raka ya pili utaamka tena na ufanye kama vile mwanzo kuanzia 3 hadi 15,halafu utaengeza 17 na halafu utainuka tena uanze tena 3 urudi 15,zitakuwa ni rakaa tatu na kama swala ni ya raka ya nne utarudi tena 3 hadi 15 kisha ile raka ya mwisho utamalizia kwanzia19 hadi 21

[2] [a]Hapo utaja ile swala unaswali [b])utataja raka zake tizama ukurasa 5

A. SURATUL FATIHA

Ni lazima mtu aijue afundishwe ama aandikiwe ili aweze kuswali na isomwe kiarabu , nayo ni;

BIsmillahi rahmani Rahim (1), Al-hamdu lillahi rwabbil Aalamin (2),Arrwahmani Rwahiim (3),
Maaliki yaumi diin (4),Iyyaka naabudu Wa iyyaka nastain (5,),Ihdina swiratwal mustaqim (6)

Swiratwal lladhina an-amta aleihim Ghairil magh-dhwubi aleihim Wallallwalliyn (7), Ameen! (Zimeandikwa kwa herufi za Kiswahili, hutamkwa hivo hivo zilivoandikwa hakubadilishwa kitu)

Hivi ndivyo inavyoandikwa kiarabu:

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ (1)
الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ (2) الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ (3) مَالِكِ يَوْمِ الدِّينِ (4) إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ (5)
اهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ (6) صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ) 7

n/b- Ni muhimu kujifunza kusoma kiarabu ili uweze kuisoma Quruani mzima, na utapa thawabu zaidi, kuna njia nyingi za kujifunza kusoma kiarabu, unaweza enda madrasa,au kutafuta mwalimu, au kutafuta program ya kujiufunza kusoma kiarabu na Quran katika simu.

B)TAHIYYATU

Ni kukaa beina ya raka mbili za mwanzo(ni sunna) nay a pili ni kukaa kabla ya kupiga salamu.

Nayo ni; "**Attahiyattu, almubaarakatu, asswala watu, attayibatu,lillah. Assalamu aleika ayyuha nnabiyu warahmatullahi wa barakatuh , assalamu aleina wa ala ibadu llahi swalihini,Ash-hadu an la ilaha illa llah wa ash-hadu anna Muhammad rasulullah.[1]Allahumma swalli ala seyyidna Muhammad wa ala aali seyyidna Muhammad, kama swalleita ala Ibrahiima wa ala aali Ibrahima fil alamina innaka hamidul majid[2] Allahumma ghfir lii min adhabil Qabri wa ghfir lii min adhabi nnar wat qiini fitnati massiyh dajjal."**

Mambo yanayovunja swala

1) Kuzungumza kwa kukusudia au kuzungumza hata kama kwa bahati mbaya au kusahau kwa maneno zaidi ya manne
2) Kula na kunywa chochote(isipokuwa mate.) kwa kukusudia, au kula chakula kingi kwa kusahau ukiwa ndani ya swala.
3) Kuvunjikiwa na udhu.
4) Kugeuka kutoka sehemu ya kibla.
5) Kufanya kitu kwa harakati (steps) tatu zilizofuatana.
6) Kuvunja nia ya kuswali.
7) Kujikohoza kohoza kusudi.
8) Kucheka (amma kutabasamu inaruhusiwa.)
9) Kulia kupita kiasi.
10) Kufungukwa na nguo mpaka ukaonekanwa uchi wako.
11) Kumtangulia imam katika nguzo mbili za swala au imaam kukutangulia kwa hizo nguzo mbili.
12) Kuacha nguzo yeyote ya swala kwa kusudi.

Swala za sunna

Hizi ni swala ambazo mtu akiswali anajikaribisha kwa mwenyezimngu, na swala hizi si lazima ila alipenda sana kuziswali Mtumi Muhammad nazo ni ;

Swala	**Nyakati**
Qabliya	Kabla kuswali faradhi
Baadiya	Baada kuswali faradhi illa alfajiri na Alasiri
Dhuha	Kuanzia kuchomoza jua kadri ya uta wa mshale hadi jua kufika kati ya mbingu
Witri	Qabla ya kulala(swala ya mwisho ya siku) Nayo ni raka zisizogawanyika kuanzia 1 hadi 11 na huswalia raka mbili mbili na kuigwa salamu baada ya kila raka 2
Swala ya kusuf na khusuf	Kushikwa jua na mwezi, swala ilio na rakaa mbili na rukuu mbili na itidaal mbili
eidayn	Swala ya edi mbili ya fitri na adh-haa
istisqai	Swala ya kuomba mvua
Tarawehe	Usiku wa ramadhani aghalabu baada ya isha

n/b-Swala za sunna ziko nyingi sana, pia kuna swala zinazoitwa nawafil nazo ni swala zisizo na idadi wala wakati maalumu kuziswali unaweza kuswali Rakaa unazotaka wewe hata kama ni elfu kumi, isipokuwa ni makruhu kuswali swala hizi au swala yoyote isiyo na sababu wakati ambao ni makruhu kuswali nazo ni:

Nyakati ambazo ni makrouh kuswali

1) Baada ya swala ya alfajiri hadi lichomoze jua
2) Jua linapochomoza hadi limalizike kuchomoza
3) Baada ya swala ya alasiri hadi juwa lizame
4) Jua linapokuwa utosini hadi lipindukie upande wa magharibi
5) jua linapozama hadi likamilike kuzama.

Mtu anapotaka kwenda kumuelekea mwenyezimungu basi ni vyema ajieke mbali na madhambi ya Viungo, na pia azidi kuomba msamaha anapomuasi mwenyezimungu kupitia viungo, mfano:

Maasi ya tumbo ni mfano:

1) Kula ribaa(hakika amelaniwa mwenye kula riba na mwenye kuchangia kuliwa ribaa)
2) Na kula vyenye kulewesha(hakika amelaniwa mwenye kunya pombe, mwenye kuuza,mwenye kubeba,mwenye kununua na yoyote yule atakae saidia katika kutengeneza na kusafirisha)
3) Na kula mali ya mayatima
4) Kula chakula cha haramu (ikiwemo alivyovikataza mwenyezimungu na vile ambavyo vimepatikana kwa njia isio halali)

Maasi ya tumbo ni mengi zaidi, unaweza kuuliza mashekhe wakuelezee zaidi.

Maasi ya ulimi ni mengi sana ikiwemo :

1. Kusengenya (kumtaja ndugu yako kwa sifa asiyoipenda hata kama ni sifa yake)
2. Kutia fitina
3. Kusema uongo
4. Kutukana
5. Kulani ..... na mengineyo

Masaasi ya jicho ni mengi sana miongoni ni:

1. Kuwatizama wanawake ajnabii (unaoruhusiwa kuwaoa na bado hujawaoa yaani wasiokuwa wale ambao hufai kuwaoa)
2. Kutizama uchi za watu
3. Kuwatizama waislamu wenzako kwa jicho la dharau
4. Kutizama ndani nyumba za watu bila ruhusa yao..... na mengineo

Maasi ya sikio pia ni mengi ikiwemo:

1. Kusikia masengenyo
2. Kusikia nyimbo za matusi na za kutukana.... na mengineyo

Maasi ya mkoni ni kama vile:

1. Kupunja watu katika kuwapimia mizani(kupunguza kiwango)
2. Kuwaonea wenzako na kuwadhulumu kupitia mkono wako.
3. Kuiba
4. Kuua
5. Kupiga bila sababu
6. Kutumia mkono wako kufanyia maasi mengineyo kama kushika wanawake au kuwasalimia kwa mkono ambao hujawaoa... na mengineyo

Maasi ya mguu ni :

1. Kuenda sehemu ya maasi
2. Kuenda sehemu kwa lengo la kumdhuru muislamu au kumua bila makosa
3. Kupiga muislamu (hata pia asiekuwa muislamu hufai kumuonea, wala kumpiga , wala kumuibia,wala kumdhuru ikiwa hana hatia- na miongoni mwa hatia ni kutangaza uadui kwa waislamu) ..... na mengineyo

Maasi ya tupu ni mengi pia kama vile:

1. Kuzini(yaani kutenda tendo la ndoa kabla ya kuoana)
2. Kufanya uliwati (yaani kustarehe kindoa kwa jinsia moja, mfano mwanamume kwa mwanamume)
3. Kujitoa mani (au punyeto au musterbation)..... na mengineyo

Na maasi ya jumla ya muili kama vile;

1. Kuwakosea wazazi wawili
2. Na kukimbia kweye vita wakati wa vita mbele ya adui wa waisilamu
3. Kukata uhusiano wa damu
4. Kutembea na kiburi hadi ukawa unaburuta nguo yako chini ya mguu.
5. Kuacha nguzo katika nguzo za kiislamu kama vile kuacha swala ya faradhi au swala ya **faradhi ya kutoshelezana** au kuacha **swala ya ijumaa**

faradhi ya kutoshelezana.

Ni aina ya faradhi ambazo waislamu wote wa mji wakikosa kuifanya basi wote watapata dhambi lakini wakifanya baadhi basi wale wengine ambao hawakufanya hawatapata dhambi.

Nazo ni:

1. Kumuosha maiti muislamu, kumvesha sanda(kumkafini), kumswalia, na kumzika.
2. Kusoma elimu yenye manufaa kwa jamii kama vile: kilimo,udaktari,tecknologia,
3. Hesabu,sayansi na mengineyo..... amma ilimu ya dini ya kujua jinsi ya kufanya ibada ni lazima kila muislamu kuisoma kabla ya kuingia kwenye ibada hio, maana yoyote atakae ifanya ibada bila kujua jinsi inavyofanywa na ikapelekea kuifanya ibada hiyo visivyo basi ibada yake haitakubaliwa na mwenyezimungu
4. Kuswali kwa jamaa(kwa pamoja) msikitini , swala ya kuswaliwa na watu kwa pamoja ni bora kulijko swala ya peke yako kwa mara 27.
5. Kuregesa salamu kwa aliesalimia.

Swala ya ijumaa

Swala ya ijumaa Ni lazima kwa kila muislamu wa kiume, mwenyeji,aliemuungwana (ambaye si mtumwa) na mwenye afya na asiekuwa na dharura za kuruhusiwa kutoswali juma.

Ijumaa ni idi ya wiki kwa hivyo ni bora kwa anae enda juma aoge, akate kucha, akate nywele za kinena(nywele za sehemu za siri), aeke wanja, atie mafuta mazuri na avae kanzu nyeupe.

Swala ya ijumaa ni raka mbili na huweko hotuba mbili kabla ya swala, na huswaliwa kipindi cha adhuhuri siku ya ijumaa.na huswaliwa kwa pamoja kwa idadi ya wanaume wasiopungua 40, ambao aghalabu huwa wamekusanyika msikitini.

n/b-Ni vizuri mtu aende mapema ilia pate thawabu nyingi, na yoyote atakaekwenda kuchelewa na akapata raka ya mwisho basi amepata swala ya ijumaa, amma akikosa raka ataswali raka nne za adhuhuri kwa sababu ijumaa litakuwa limeshampita.
Maelezo zaidi ya swala ya ijumaa na swala zile nyengine maalumu tutazielezea katika kitabu cha toleo la pili in sha Allah apendapo Mwenyezimungu.

- Waisamu ni bora wakusanyike katika msikiti mmoja kuswali ijumaa ambao kwa kila mji huwa msikiti huo unaitwa Jamiah au msikiti wa ijumaa, isipokuwa kama msikiti uko mbali au umejaa na miskiti mengine ipo basi ataswali miskiti hio mengine
- Pia aangalie ni msikiti gani utakuwa na hotuba ya manufaa badala ya kwenda mikiti ambayo kawaida yake ni kutukana na kukejeli waislamu wenzao katika hotuba zao.

Sababu ambazo zinamruhusu muislamu kukosa swala ya ijumaa au swala ya jamaa.

1. Mvua kubwa ya mafuriko
2. Upepo mkali wenye kutishia maafa
3. Njaa kali na kiu kwa alieekewa chakula wakati wa swala
4. Ubaridi au joto kali la kuhatarisha maisha ya ataake toka
5. Kuanguka kwa kuta barabarani kuelekea msikitini
6. Mitetemeko ya ardhi
7. Kumomonyoka kwa udongo hatari(erossion)
8. Kuanguka theluji nyingi zenye kutishia kuhatarisha maisha

9. Maradhi ambayo yamemshinda kufika msikitini

10. Anaekaa na mgonjwa mahututi kadri akiondoka mgonjwa atapata shida au mgonjwa anakaribia kufa na anaogopa anaeza enda ijumaa na akija akawa ameshafariki

11. Kuogopea kupoteza mali zake au familia yake au cheo chake lau ataenda msikitini, kwa sababu mzito fulani.

12. Kukosa nguo yake ya heshima aliozoeleka kuvaa kila mahala.

13. Kuogopa kuenda msikitini kwa sababu ya deni aliokuwa nalo na anajitahidi kulipa lakini hajaweza kulipa na anaogopa kuwa lau ataenda ijumaa mwenye deni atamuaibisha,

n/b kwa sababu zote hizi na nyenginezo basi mtu ataswali nyumbani na hatopata ndambi ya kutoswali jamaa , amma ikiwa ni swala ya Ijumaa basi ataswali nyumbani tuh rakaa nne za adhuhuri badala ya ijumaa

Mwisho

Hapa ndio itakuwa mwisho wa kitabu hiki kidogo na in sha Allah natarajia kitakuwa na manufaa kwako na yoyote yule utakaempa kusoma au ukamsomesha.

Huenda kukawa kuna makosa kidogo ambayo imma ni ya ki uchapishaji au kukosekana neno Maalumu kwa kupitia uchache wa ilimu yangu au makosa ya mitambo.

Pia naomba radhi kwa makosa ambayo yanaweza yakaonekanwa kuwa ni maneno ya kejeli au au kumgusa mtu,au kushindana na mtu. Hio itakuwa ni kuelewana vibaya tuh lakini sio makusudio ya hiki kitabu.

kitabu hiki nimekiandika mwaka wa 2017 na kukificha nikiogopea uchache wa ilimu yangu(nikiwa na umri wa miaka 19 , na baadae nimeamua kujipa moyo na kukitoa mbele za watu baada ya miaka 7...

Nimekitoa mwaka huu tarehe 14- SEP- 2023 , sawia na tarhe 28-Swaffar– 1445 H

Nimepata moyo wa kukitoa baaada ya kumuona mwenzangu Sharif Muhammad Khatwab Kijana kama mimi kuwa ametoa kitabu mfano wa kitabu hiki anachoikiita **YANAYOMLAZIMU KILA MUISILAMU**. Kitabu ambacho ni kizuri na nahimiza anaesoma hiki kitabu changu akitafute na hiki cha sharif Muhammad aliekitoa siku moja kabla ya mimi kukitoa hiki changu,amekitoa tarehe 13- Sep-2023.

NI mimi mtumishi wenu :

Almufatish

Ustadh Ali Alhaidary – Malindi kenya

Anwani: haidarkindy@gmail.com

Natarajia mawasiliano na taaliqi yoyote kutoka kwa aliejaliwa kusoma kijitabu hiki.Shukran.

Kitabu hiki cha " Mti wa dini zawadi kwa walioongoka katika dini" ni kijitabu kidogo nilichokusudia Muhtadeen yaani waongofu ambao wanataka kujua ilimu yao ya dini ili waweze kumuabudu mwenyezimungu anavyostahiki kuabudiwa.

Natarajia atakae kisoma kijitabu hiki na kukielewa basi atakuwa ni miongoni mwa wale wenye ufahamu kwenye dini na ataweza kuwasomesha na wenzake haswa wale ambao wamesilimu karibuni na hawajapata nafasi ya kuijua dini yao ki ukamilifu haswa upande wa ibada

ilimu ya dini ya kujua jinsi ya kufanya ibada ni lazima kila muislamu kuisoma kabla ya kuingia kwenye ibada hio, maana yoyote atakae ifanya ibada bila kujua jinsi inavyofanywa na ikapelekea kuifanya ibada hiyo visivyo basi ibada yake haitakubaliwa na mwenyezimungu.